# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA RAIS

Simu ya Upepo **“SEKRETARIETI”**
Simu: 255 (026) 2963652
Tovuti: **www.ajira.go.tz**
Barua:Pepe:**katibu@ajira.go.tz**

Sekretarieti ya Ajira katika
Utumishi wa Umma,
Jengo la Utumishi (UDOM) na
Eneo la Dkt. Asha Rose Migiro,
S. L. P. 2320,
**DODOMA.**

## TANGAZO

**31.10.2024**

**MABADILIKO YA MAHALI PA KUFANYIA USAILI WA KUANDIKA KWA NJIA YA MTANDAO (OATS) CHUO CHA USIMAMIZI WA FEDHA (IFM)**

Wasailiwa wote waliopangiwa kufanya usaili katika **Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM) – Dar es Salaam** kwa **tarehe 01 na 04 Novemba, 2024** mnajulishwa kuwa kuna mabadiliko ya mahali pa kufanyia usaili wa kuandika kwa njia ya mtandao (online).

Usaili wa Kuandika kwa njia ya mtandao ( online) **kwa tarehe 01/11/2024 na tarehe 04/11/2024** utafanyika katika **Chuo Kikuu cha Mtakatifu Joseph (SJUIT)** kilichopo **Mbezi, Jijini Dar es salaam** badala ya **Chuo cha Usimamizi wa Fedha ( IFM )** kama ilivyoonekana katika akaunti zenu hapo awali.

Aidha, wasailiwa waliopangiwa kufanya usaili **tarehe 02/11/2024 na tarehe 03/11/2024** katika **Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM) - Dar es Salaam mnajulishwa kuwa hakutakuwa na mabadiliko yoyote ya mahali pa kufanyia usaili.**

Vilevile, muda wa usaili utabaki kama ulivyo kwenye tangazo la awali la kuitwa kwenye usaili. Kwa taarifa zaidi tembelea tovuti yetu www.ajira.go.tz pamoja na akaunti yako ya Ajira Portal kuona mabadiliko hayo.

Beatrice Kimwaga
Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini.